JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

## IDARA YA MISITU NA NYUKI

**MWONGOZO WA UVUNAJI KATIKA MISITU YA HIFADHI YA VIJIJI**




Umetayarishwa na Kampeni ya Mama Misitu kwa niaba ya Idara ya Misitu na Nyuki

Dar es Salaam
Oktoba 2015

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

## IDARA YA MISITU NA NYUKI

**MWONGOZO WA UVUNAJI KATIKA MISITU YA HIFADHI YA VIJIJI**

Umetayarishwa na Kampeni ya Mama Misitu kwa niaba ya idara ya Misitu na Nyuki

Dar es Salaam,
Oktoba 2015

## Dibaji

Tafsiri rahisi ya mwongozo wa uvunaji katika misitu ya hifadhi ya vijiji umetafsiriwa kutoka kwenye kitabu kilichotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii mwaka 2013. Kutokana na mwongozo huo kuandaliwa katika lugha ya kiingereza, Idara ya Misitu na Nyuki kwa kushirikiana na Kampeni ya Mama Misitu imeratibu utengenezaji wa tafsiri rahisi ya mwongozo wa uvunaji katika misitu ya hifadhi ya vijiji ili kuongeza ushiriki wa jamii hasa za vijijini katika kutekeleza mipango ya uvunaji endelevu katika maeneo yao.

Kijitabu cha mwongozo wa uvunaji katika misitu ya hifadhi ya vijiji kitasaidia kamati za maliasili, Serikali za vijiji, Halmashauri za Wilaya, Asasi za kiraia, wafanyabiashara wa mazao ya misitu na wananchi kwa ujumla kufahamu kazi na majukumu yao katika kuwezesha uvunaji endelevu na wenye manufaa kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Idara ya Misitu na Nyuki inatoa shukrani kwa wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika uandaaji na uboreshaji wa tafsiri hii rahisi ya mwongozo wa uvunaji katika misitu ya hifadhi ya vijiji. Kipekee, tunatoa shukrani kwa Kampeni ya Mama Misitu kwa kuwezesha uchapishaji wa kijitabu hiki.

Tumerithi. Tuwarithishe!

Gladness Mkamba
Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Misitu na Nyuki,
Wizara ya Maliasili na Utalii
2015

## Utangulizi

Chini ya Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002, jamii inaweza kulinda, kuhifadhi, kusimamia na kutumia kiundelevu misitu katika ardhi ya kijiji ili kukidhi mahitaji yao ya kimaendeleo ya muda mrefu. Mpaka sasa, zaidi ya hekta milioni 2 za misitu zinasimamiwa na serikali za vijiji zaidi ya elfumoja nchini kote. Jamii zinazosimamia misitu hii zina shauku ya kujua jinsi wanavyoweza kunufaika kutokana na uvunaji endelevu.

Kijitabu hiki kinatoa mwongozo juu ya jinsi misitu kwenye ardhi ya kijiji inavyoweza kuvunwa kwa njia endelevu na kunufaisha jamii vijijini. Mwongozo huu unazilenga kamati za maliasili za vijiji kundi ambalo hupanga mipango ya uvunaji endelevu katika misitu ya vijiji vyao na linalohitaji ushauri wa jinsi ya kufanya hivyo. Halmashauri za wilaya pia zinaweza kufaidika kutokana na mwongozo wa kisheria katika kijitabu hiki.

Mwongozo huu umegawanyika katika hatua kuu mbili. Hatua ya kwanza inaeleza kuhusu kuanzisha na kutangazwa msitu wa hifadhi wa kijiji na hatua ya pili inahusu maandalizi ya uvunaji katika msitu wa hifadhi wa kijiji.

## Hatua ya Kwanza:

## KUANZISHA NA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI WA KIJIJI

Mambo muhimu katika hatua hii ni kama yafuatavyo:

1. Kuchagua Kamati ya Maliasili ya Kijiji




2. Kubainisha na kutenga eneo la msitu/pori katika ardhi ya kijiji



3. Kufanya Tathmini Shirikishi ya Rasilimali ya msitu kubaini ujazo na aina ya miti inayoweza kuvunwa katika eneo lililotengwa  kwa ajili ya uvunaji.

4. Kuandaa na kupitisha mpango wa usimamizi ambao unahusisha mpango wa uvunaji

5. Kuandaa sheria ndogo za kusaidia utekelezaji wa mpango wa usimamizi na kuziwasilisha katika Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya kupitishwa.

6. Mkutano Mkuu wa Kijiji unatamka msitu wa hifadhi wa kijiji

7. Msitu wa Kijiji unaweza ama kusimamiwa na kijiji kimoja - au katika baadhi ya matukio, ambapo msitu unamilikiwa kwa pamoja na vijiji vingi - unaweza kusimamiwa kwa pamoja na kamati inayoundwa na wawakilishi wa vijiji vyote.

8. Wilaya inasajili Msitu wa hifadhi wa kijiji katika daftari la usajili wa misitu ya Hifadhi ya Vijiji.

9. Msitu unaweza kutangazwa katika gazeti la serikali na Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki - lakini hii si lazima. Serikali za vijiji zinaweza kuendelea kusimamia na kuvuna misitu bila kupitia hatua hii ya ziada.

## Hatua ya pili:

## MAANDALIZI YA UVUNAJI

Mara baada ya kukamilisha mambo yaliyopo katika hatua ya kwanza kijiji kinaweza kuanza kufikiri juu ya maandalizi kwa ajili ya kuvuna na kutumia msitu. Katika baadhi ya maeneo uvunaji wa msitu hauwezekani kwa kipindi fulani ili kupisha ukuaji wa miti na urejeshaji wa uoto kabla ya kufanya uvunaji. Kwa sababu hiyo, ni jambo la kawaida kwa mpango wa usimamizi na sheria ndogo za misitu mingi zikatokana na uhifadhi, ulinzi na mara nyingi kuzuia uvunaji wa aina yoyote kufanyika. Mara baada ya miti kufikia ukubwa unaofaa kuvunwa, itakuwa muhimu kupitia na kurekebisha mpango wa usimamizi na sheria ndogo ili kuhakikisha kuwa uvunaji unaingizwa katika mpango.

Hatua muhimu zifuatazo zinahitaji kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba uvunaji katika Misitu ya Hifadhi ya Kijiji unaendana na sheria ndogo na mpango wa usimamizi wa msitu

1. Sheria inataka kila kijiji kipate nyundo ya uvunaji. Vijiji vinaweza kuomba nyundo yao kutoka Idara ya Misitu na Nyuki kupitia Halmashauri ya Wilaya yao, na nyundo hii itatumika kisheria katika kuweka alama katika mbao zilizovunwa kiuendelevu kutoka katika msitu wa kijiji. Kwa kuwa upatikanaji wa nyundo unaweza kuchukua muda mrefu, kijiji kinaweza kumwomba Afisa Misitu wa Wilaya kutumia nyundo ya Halmashauri ya Wilaya kuweka alama mbao zilizovunwa kwenye Msitu wa Hifadhi wa Kijiji. Gharama za kutumia nyundo ni lazima zilipwe na mnunuzi wa mbao na siyo mameneja wa misitu ya vijiji.

2. Kamati ya Maliasili ya Kijiji, pamoja na Afisa Msitu Wilaya kutambua na kuweka alama katika miti yenye ukubwa wa kuvunwa – kwa kuzingatia mpango wa uvunaji - na katika vitalu maalum.



**Kama idadi ya miti ya kuvunwa ni kubwa (kwa mfano zaidi ya miti 50) fuata hatua ya 3 - 6 Kama ni kiasi kidogo cha mbao (Miti michache tu) fuata hatua ya 7.**

**Aidha...**

3. Kamati ya Maliasili ya Kijiji, pamoja na Afisa Misitu Wilaya na ikiwezekana kwa msaada kutoka kwa Idara ya Misitu na Nyuki, kutangaza tenda au kuwaalika wavunaji wenye nia ya kuvuna miti iliyotayari kuvunwa. Idara ya Misitu na Nyuki inaweza kusaidia katika kubaini ikiwa ni wavunaji hao ni waadilifu na hawana migogoro ambayo haijatatuliwa na serikali

4. Wavunaji walioteuliwa wanakaribishwa kuona miti na kuwasilisha kijijini zabuni zilizofungwa kwa kuzingatia idadi ya miti waliokubaliana, au ujazo utakaovunwa. Zabuni zilizopokelewa zisibainishe tu kiasi cha fedha kitakacholipwa kwa ujazo wa mbao bali ziainishe pia faida nyinginezo ambazo wanakijiji watazipata (ikiwamo matumizi ya bure ya mabaki ya miti kwa ajili ya uchomaji mkaa, ajira kwa wanakijiji, uboreshaji wa barabara, na kadhalika).

5. Zabuni zilizofungwa zitafunguliwa katika mkutano wa kijiji na kwa misingi hii, uamuzi juu ya mzabuni wa kuvuna mazao husika unafanyika na kuwasilishwa kwenye Serikali ya kijiji kwa ajili ya kupitishwa. Maelezo yote ya wazabuni na zabuni zilizoshinda zinawekwa kwenye ubao wa matangazo wa kijiji.




6. Mvunaji au wavunaji walioshinda watapewa taarifa na hufanya malipo ya awali (Kama vile asilimia 50% ya gharama za mrabaha - au kama ilivyokubaliwa katika mkataba) na anapewa leseni ya kuvuna mbao kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

## Au...

7. Kuhakikisha kwamba mvunaji wa mbao anapata leseni ya uvunaji miti iliyokusudiwa ndani ya eneo la uvunaji na analipa mrabaha unaolingana na viwango vya soko.

## Kisha....

8. Fedha zote lazima zikatiwe stakabadhi na Kamati ya Maliasili ya Kijiji na kisha ziingizwe kwenye akaunti iliyotengwa kwa ajili ya usimamizi wa msitu.

9. Uvunaji unafanyika chini ya usimamizi wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji ili kuhakikisha unazingatia mpango wa uvunaji na kiasi kilichokubalika kukatwa. Baada ya kuvuna mbao zinagongwa alama ya nyundo ya kijiji/ Halmashauri ya Wilaya na ya mnunuzi.

10. Afisa Msitu Wilaya atatoa hati ya kupita kuruhusu usafirishaji wa mbao (ikiwa zinakwenda nje ya wilaya) kwa kuzingatia uthibitisho wa mbao zilizovunwa na kibali cha uvunaji.


11. Asilimia tano (5%) ya mrabaha hulipwa na mvunaji kama ushuru kwa serikali za mitaa.

12. Mfanyabiashara kuondosha magogo na kuyapeleka kwenye kiwanda cha kupasua mbao kwa ajili ya uchakataji na kuuza.



Muhtasari wa hatua zote za uvunaji umeonyeshwa hapa chini. Sehemu ya njano inaonesha hatua zinazohitajika kwa ajili ya jamii kutangaza na kusimamia kisheria msitu wao wenyewe - na sehemu ya kijani inaonesha hatua zinazotakiwa ili kuvuna msitu kwa uendelevu.

## Muhtasari wa hatua za kisheria za kuanzisha msitu wa hifadhi wa kijiji hadi kuvuna



## Maelezo ya ziada

1. Uvunaji katika msitu wa kijiji ulioidhinishwa na Baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya hauhitaji kujadiliwa na Kamati ya Uvunaji ya Wilaya ilimradi haupingani na mpango wa usimamizi uliopitishwa na sheria ndogo.

2. Mapato yatokanayo na uvunaji katika misitu ya hifadhi ya vijiji yanaweza kubakizwa asilimia yote mia moja (100%) katika halmashauri ya kijiji.

3. Halmashauriya kijiji, kama ngazi ya juu ya serikali katika kijiji itafanya maamuzi juu ya kiasi cha mapato ambacho kitarejeshwa katika shughuli za usimamizi wa misitu (kama vile kufanya ulinzi katika mipaka ya msitu, ufuatiliaji, na manunuzi ya vifaa mbalimbali n.k. ) na kiasi gani kitatumika kwa maendeleo kulingana na vipaumbele vya kijiji (kama afya, elimu). Ni muhimu mgawanyo huo uoneshwe kwenye mpango wa usimamizi wa msitu.

4. Vijiji havipaswi kugawana mapato yao na Serikali kuu au Halmashauri ya Wilaya, isipokuwa tu ushuru wa kawaida. Baadhi ya Vijiji vimeridhia kuipatia halmashauri ya wilaya kiasi kidogo cha mapato kwa ajili ya kukidhi huduma iliyotolewa na ofisi ya misitu ya wilaya. Kwa kawaida, hii ni kati ya asilimia 10 – 15 ya jumla ya maduhuli yaliyokusanywa.

# Kampeni ya Mama Misitu

Mama Misitu ni Kampeni ya mawasiliano inayolenga kuboresha utawala wa Misitu Tanzania, na kukuza matumizi endelevu ya mazao ya Misitu ili watu wa Tanzania wanufaike zaidi na rasilimali za Misitu. Kampeni ya Mama Misitu imebeba dhamira na maono ya kuhifadhi, kulinda na kuhamasisha matumizi endelevu ya Misitu. Kampeni ya Mama Misitu inatekelezwa na kikundi kazi cha misitu Tanzania na kuratibiwa na Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF).

LAWYERS ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)
SHERIA NA ULINZI WA MAZINGIRA

JOURNALISTS ENVIRONMENTAL ASSOCIATION OF TANZANIA

TRAFFIC
the wildlife trade monitoring network

Femina HIP

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA
MJUMITA

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Mpingo Conservation & Development Initiative

policy forum

Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

# Tumerithi




# Tuwarithishe

Kampeni ya Mama Misitu, Namba 27 Mtaa wa Sangara - Mikocheni, Dar es Salaam. | **Tovuti:** www.mamamisitu.com | **Barua pepe:** info@mamamisitu.com | **Simu:** +255 758828398 | **Facebook:** www.facebook.com/mamamisitu | **Twitter:** www.twitter.com/mamamisitu

Uandaaji na uchapishaji wa mwongozo huu pamoja na Kampeni ya Mama Misitu vimefadhiliwa na Serikali ya Ufini.

FORMIN.FINLAND.FI

MINISTRY FOR FOREIGN
AFFAIRS OF FINLAND